UTEKELEZAJI>>Rais

Jumatatu Desemba 15, 2025

# LATRA yatoa vibali 158 kwa mabasi ya mikoani

Na REHEMA MAIGALA

MAMLAKA ya Udhibiti Usafiri Ardhini (LATRA), imetoa vibali vya usafiri 158 vya mabasi yanayotoka Dar es Salaam kwenda mikoa mbalimbali, kuondoa changamoto ya usafiri kipindi cha sikukuu za mwisho wa mwaka.

Akizungumza na gazeti hili Dar es Salaam, jana, Ofisa Mfawidhi wa LATRA Kituo cha Mabasi cha Magufuli, Rukia Kibwana, alisema vibali hivyo vya muda hutolewa mwisho wa mwaka kutokana na ongezeko kubwa la abiria wanaosafiri kwenda mikoani.

Rukia alisema hadi kufikia jana mchana vibali 158 vilitolewa kwa mabasi yaendayo mikoa yote nchini.

"Hadi leo (jana) mchana tulitoa vibali 158 ambapo usafiri mwingi ni jioni, unapoona watu wamejaa stendi wanakuja kusubiri mabasi yao na wengine wanawahi kukata tiketi," alisema.

Rukia alisema awali walianza kutoa vibali 72 kwa mikoa mitano ambayo ilionekana ina abiria wengi

> **Hivi sasa tumetoa vibali 158 katika mikoa yote ya Tanzania, kufanya hivi tumepunguza msongamano wa abiria wakati wa asubuhi na jioni.**
>
> Rukia Kibwana.

ambayo ni Dodoma, Iringa, Tanga, Morogoro na Kilimanjaro.

"Hivi sasa tumetoa vibali 158 katika mikoa yote ya Tanzania, kufanya hivi tumepunguza msongamano wa abiria wakati wa asubuhi na jioni,"aliongeza.

Rukia aliwataka wananchi kuwa na uvumilivu kipindi cha mwisho wa mwaka, akieleza LATRA inafahamu idadi kubwa ya watu husafiri kwenda mikoani, hivyo inaendelea kusimamia na kuratibu uongezaji wa mabasi kadri inavyohitajika.

"Kipindi cha kuelekea sikukuu za mwisho wa mwaka Krismasi na mwaka mpya, baadhi ya wananchi wanapenda kusafiri kwenda kusheherehekea na familia zao,"alisema.

LATRA imekuwa na utaratibu wa kutoa vibali vya muda kinapofika kipindi cha msimu wa sikukuu, lengo ni kuhakikisha upatikanaji wa usafiri unakuwa wa uhakika.